JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

Anwani ya Simu:"TAMISEMI"
DODOMA
Simu Na : 026-2322848,
2321607, 2322853,
Fax: 026-2322116, 2322146
Email Address: ps@pmoralg.go.tz
Unapojibu tafadhali taja:

Tawala za Mikoa na
Serikali za Mitaa,
S.L.P. 1923,
DODOMA.

Kumb. Na. HB.81/116/01/42 20 Desemba, 2010

OFISI YA MKUU WA MKOA
13 JAN 2011
S.L.P. 5095 TANGA

HALMASHAURI YA WILAYA
IMEPOKELEWA
26/1/2011
TAREHE
HANDENI

Makatibu Tawala wa Mikoa,
**TANZANIA BARA.**

## WARAKA NA 2 WA MWAKA 2010

## USHIRIKISHWAJI WA OFISI YA MKUU WA WILAYA KATIKA MIKUTANO NA VIKAO VYA HALMASHAURI

### 1.0 Utangulizi:

1.1 Serikali imekuwa inatekeleza mageuzi makubwa katika mfumo na muundo wa Serikali kuhusiana na mgawanyo wa madaraka, majukumu na raslimali kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Katika kutekeleza mageuzi hayo, Serikali ilitoa Sera ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa ya mwaka 1998 ambayo inalenga kuimarisha utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutoa huduma bora kwa wananchi kwa ufanisi zaidi.

1.2 Ili kutekeleza Sera hiyo, Sheria mbalimbali za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa zimekuwa zinafanyiwa marekebisho kwa madhumuni ya kuzifanya ziendane na Sera ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa. Moja ya matakwa ya Sera hii ni umuhimu wa kuwashirikisha wananchi na asasi zisizo za Kiserikali katika Upangaji, Usimamizi na Utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo.

1.3 Katika kutekeleza matakwa ya Sera ya kuwashirikisha wananchi katika kuamua, kupanga, kusimamia na kutekeleza mipango inayohusu maendeleo yao, mwaka 2006, Bunge lilipitisha marekebisho ya Sheria za Serikali



Scanned by CamScanner

za Mitaa Sura 287 na 288 na Sheria ya Tawala za Mikoa Sura 97 kwa Sheria Namba 13/2006 ambayo pamoja na mambo mengine ilianzisha Kamati ya Mashauriano ya Wilaya (DCC) ambayo iko chini ya Uenyekiti wa Mkuu wa Wilaya na Katibu wake ni Mkurugenzi wa Halmashauri.

1.4 Jukumu Kuu la Kamati hii ni kupokea taarifa za miradi na programu za Maendeleo na kuzitolea maoni na ushauri kwa lengo la kuboresha uekelezaji wa miradi hiyo ambayo kwa kiasi kikubwa hutekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika ngazi mbalimbali na Mashirika ya Umma, Vyama vya Ushirika na Asasi zisizo za Kiserikali.

## 2.0 Kasoro zilizojitokeza:

2.1 Uzoefu uliopatikana unaonesha kuwa, ingawa Kamati ya Mashauriano ya Wilaya (DCC), inashughulikia masuala ya maendeleo na utoaji wa huduma ambao hufanywa na Halmashauri, hakuna uwakilishi wa kiutendaji wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya katika mikutano ya timu ya Menejimenti, Vikao vya Baraza la Halmashauri na hivyo kuikosesha Ofisi ya Mkuu wa Wilaya taarifa za kila wakati kuhusu mwenendo wa utekelezaji wa mipango, miradi ya Maendeleo na uendeshaji wa kazi na majukumu ya Halmashauri.

2.2 Ukosefu wa taarifa unamfanya Mkuu wa Wilaya ashindwe kutekeleza wajibu wake wa kuzisimamia kikamilifu Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutekeleza majukumu yake. Mkuu wa Wilaya kama ilivyo kwa Mkuu wa Mkoa anao wajibu wa kusimamia utekelezaji wa kazi na shughuli zote za Serikali katika Wilaya anakofanyia kazi. Pale inapotokea kuna kasoro katika utekelezaji wa shughuli za Serikali, Mkuu wa Wilaya hulazimika ama kuchukua hatua yeye mwenyewe au kutoa taarifa kwa Mkuu wa Mkoa na kumshauri ili achukue hatua zinazostahili. Hata hivyo, hataweza kutimiza wajibu huu kama hatakuwa na mfumo wa kuelewa kinachoendelea katika Halmashauri zilizo ndani ya Wilaya anakofanyia kazi. Hivyo, imeamuliwa kuwa utaratibu uliopo ufanyiwe marekebisho ili kuipatia fursa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kuelewa kinachoendelea kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. **Imeamuliwa kuwa, Makatibu Tawala wa Wilaya wawe wanaalikwa kwenye**



Scanned by CamScanner

**Vikao vya Timu ya Menejimenti na Mabaraza ya Madiwani (*Full Council*).**

## 3.0 Utaratibu mpya:

3.1 Utaratibu huu mpya utamuwezesha Mkuu wa Wilaya akiwa ni Kiongozi Mkuu wa Serikali Wilayani, kuwa na mfumo rasmi wa kupata taarifa za kila wakati za mwenendo wa uendeshaji na utendaji kazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taarifa zinazotakiwa ni za shughuli zote zinazotekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuhusu mipango, miradi na shughuli mbalimbali zilizopangwa kutekelezwa na mwenendo mzima wa utekelezaji na matokeo yake. Aidha, Waraka huu utasaidia kutoa ufumbuzi wa baadhi ya matatizo yaliyopo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa hivi sasa kwa kuimarisha utendaji, uwazi na uwajibikaji miongoni mwa watumishi wa umma na wawakilishi wa wananchi. Kwa Waraka huu inaelekezwa kwamba;

3.1.1 Katibu Tawala wa Wilaya (DAS) atakuwa Mualikwa katika vikao vyote vya Menejimenti ya Halmashauri (i.e *Council Management Team*);

3.1.2 Katibu Tawala wa Wilaya (DAS) atakuwa mualikwa katika vikao vyote vya Baraza la Madiwani (*Full Council*);

3.1.3 Katibu Tawala wa Wilaya atawajibika kutoa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya kuhusu mwenendo wa utekelezaji wa shughuli mbalimbali zilizopangwa kutekelezwa na Halmashauri;

3.1.4 Katibu Tawala wa Wilaya atahakikisha kuwa Mkuu wa Wilaya anapata taarifa za fedha na rasilimali nyinginezo kila zinapotumwa katika Halmashauri na kumfafanulia madhumuni ya fedha/raslimali hizo;

3.1.5 Taarifa mbalimbali atakazopata Katibu Tawala wa Wilaya kutokana na ushiriki wake katika vikao vilivyotajwa hapo juu, zinaweza kutumiwa kuandaa safari za kikazi zilizotengewa fedha katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ndani ya Wilaya yake.



Scanned by CamScanner

3.1.6 Pale itakapobainika kuwa, Halmashauri haitekelezi majukumu yake ipasavyo, Katibu Tawala wa Wilaya atawajibika kumtaarifu Mkuu wa Wilaya vilivyo ili achukue hatua zifaazo.

3.2 Ikiwa itabainika kuwa Katibu Tawala wa Wilaya hakumpatia Mkuu wa Wilaya taarifa muhimu kuhusu utekelezaji usioridhisha wa mipango na shughuli za Halmashauri, basi, hatua za nidhamu zitachukuliwa dhidi yake kwa kushindwa kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa maelekezo ya Waraka huu.

**4.0 Hali ya kipekee ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam:**

Kwa upande wa Halmashauri ya Jiji la Dar Es Salaam, Katibu Tawala wa Mkoa atamteua mmoja wa Makatibu Tawala Wasaidizi (AAS) awe anahudhuria vikao vya timu ya Menejimenti ya Halmashauri ya Jiji pamoja na Kamati zinazohusika na kumpatia Katibu Tawala wa Mkoa taarifa ambazo atazitumia katika kumshauri Mkuu wa Mkoa wa Dar Es Salaam.

**5.0 Hitimisho:**

Makatibu Tawala wa Mikoa mnatakiwa kuyafikisha maelekezo haya kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri zilizomo katika Mikoa yenu na kusimamia utekelezaji wa maelekezo haya. Aidha, Makatibu Tawala wa Mikoa mnaelekezwa kuwapatia Makatibu Tawala wa Wilaya taarifa kuhusu fedha zinazoletwa kwenye Halmashauri ili kuwawezesha kushiriki vizuri katika vikao husika kutokana na kufahamu kiasi cha fedha kilichopokelewa katika Halmashauri zilizomo kwenye Wilaya zao na kumfahamisha Mkuu wa Wilaya vilivyo.

**6.0 Kuanza kutumika kwa Waraka:**

Waraka huu unaanza kutumika tarehe 03 Januari, 2011.

Tarishi, M.K.
**KATIBU MKUU**



Scanned by CamScanner